# EE BABA MIKONONI MWAKO

MWECAU

18 April 2019

Jackson Mbena




1. Nimekukimbilia wewe Bwana, nisiaibike milele, kwa haki yako uniponye//
   Mikononi mwako naiweka roho yangu, umenikomboa, Ee bwana Mungu wa kweli.

2. kwa sababu ya watesi wangu nimekuwa laumu, naam, hasa kwa jirani zangu//
   Na kitu cha kutisha kwa rafiki zangu, walioniona njiani walinikimbia.

3. Nimesahauliwa kama mtu asiyekumbukwa, nimekuwa kama chombo kilichovunjika//
   Maana nimesikia masingizio ya wengi, hofu ziko pande zote.

4. Lakini mimi nakutumaini wewe Bwana, nimesema, wew ndiwe Mungu wangu//
   Nyakati zangu zimo mikononi mwako, uniponye na adui zangu, nao wanaonifuatia.

5. Umwangaze mtumishi wako, kwa nuru ya uso wako, uniokoe kwa ajili ya fadhili zako//
   Iweni hodari, mpige moyo konde, ninyi nyote mnaomngoja Bwana.

@ Mwenge Catholic University 2019